# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA ISHIRINI NA MBILI

**12 MEI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

___________________

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA ISHIRINI NA MBILI – TAREHE 12 MEI, 2025

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## III. MASWALI:

## OFISI YA WAZIRI MKUU:

**274 MHESHIMIWA GRACE VICTOR TENDEGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha Watu wenye Ulemavu wanajikwamua kimaisha.

**275 MHESHIMIWA MARYAM AZAN MWINYI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukomesha vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa Wafanyakazi wa Majumbani unaozidi kukithiri kwenye Jamii.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**276 MHESHIMIWA MINZA SIMON MJIKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka Magari ya Wagonjwa katika Vituo vya Afya Ilamba Ndogo na Mwasengela - Meatu.

**277 MHESHIMIWA ROBERT CHACHA MABOTO (BUNDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kumaliza ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Bunda.

**278 MHESHIMIWA JOSEPH GEORGE KAKUNDA (SIKONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itafikisha huduma za maji safi na salama katika Shule zote za Msingi na Sekondari nchini.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**279 MHESHIMIWA TOUFIQ SALIM TURKY (MPENDAE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, kuna mpango gani kutatua changamoto za NEMC hususan za kibajeti ili iweze kushughulikia athari zitokanazo na uchafuzi wa mazingira nchini.

**WIZARA YA NISHATI:**

**280 MHESHIMIWA TWAHA ALLY MPEMBENWE (KIBITI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, kuna mkakati gani wa kutatua tatizo la kukatika kwa umeme katika Jimbo la Kibiti.

**WIZARA YA MAJI:**

**281 MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA (NANYAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini ukarabati na upanuzi wa Mradi wa Maji Makonde utakamilika.

**282 MHESHIMIWA NASHON WILLIAM BIDYANGUZE (KIGOMA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itakamilisha Miradi ya Maji ya Rukoma na Mwakizega - Uvinza.

**WIZARA YA UCHUKUZI:**

**283 MHESHIMIWA NEEMA GERALD MWANDABILA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, Serikali imetoa fedha kiasi gani za ujenzi wa Bandari Kavu katika Mji wa Tunduma ambayo ni muhimu katika kukuza uchumi wa Taifa.

**284 MHESHIMIWA JANETH ELIAS MAHAWANGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, kuna Sera za Vipaumbele kwa ajili ya Wanawake Wajasiriamali katika miradi ya usafirishaji ya Serikali.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**285 MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itaweka uzio katika Hifadhi za Taifa ili kunusuru maisha ya Wananchi na mali zao dhidi ya Wanyamapori.

**WIZARA YA AFYA:**

**286 MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (BLW):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, kwa kiasi gani huduma za Utengamao zitolewazo na Wizara ya Afya zinasaidia Watu wenye Ulemavu kumudu maisha na kuleta maendeleo.

**WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**287 MHESHIMIWA FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itakomesha wizi wa mtandao kupitia *Sim banking* na ni Wahalifu wangapi wamekamatwa na hatua gani zimechukuliwa.

**WIZARA YA UJENZI:**

**288 MHESHIMIWA FLORENT LAURENT KYOMBO (NKENGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Katoma – Bukwali yenye urefu wa Km 35 utakamilika.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**DODOMA**
**12 MEI, 2025**

**BARAKA I. LEONARD**
**KATIBU WA BUNGE**